



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI GEITA



Kumb. Na. AB.55/451/01/65

TAREHE: 13/01/2023

## YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita anawatangazia wananchi wote nafasi za ajira ya kudumu kwa kada ya Watendaji wa Mitaaa kama ifuatavyo.

### 1.0 MTENDAJI WA MTA A DARAJA III - NAFASI MBILI (02)

#### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kusimamia na kutekeleza sheria ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- Kushauri kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya maendeleo katika Mtaa.
- Kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
- Kusimamia na kutekeleza mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa.
- Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.

#### 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI:

- i. Mwombaji awe na Elimu kidato cha Nne (IV) au sita (VI).
- ii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- iii. Awe na Umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 45.
- iv. Awe ni raia wa Tanzania.

**1.3 MSHAHARA:**

Ngazi ya Mshahara ni **TGS B.**

**NB:** Mtumishi atakayeajiriwa hataruhusiwa kuhama kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu (3) tangu tarehe yake ya ajira.

**UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI**

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **26/01/2023** saa **9:30** Alasiri. Maombi yatumwe kwa njia ya Posta kwa **S.L.P 384, Geita** au yaletwe Masjala ya Halmashauri ya Mji Geita, watakaokidhi vigezo watajulishwa kwa simu na katika mbao za matangazo ili kuweza kuja kwenye usaili.

Tangazo hili limetolewa na,



*Egidy Teulas,*  
**KAIMU MKURUGENZI WA MJI.**

**MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA M  
GEITA.**